

Ndugu waheshimiwa, wapendwa wanafunzi na marafiki zetu,
Baada ya salamu nyingi ni furaha yetu kubwa kutangaza kikao kifuatacho cha

Baraza letu la Kiswahili la Berlin (BALAKI-BE) la tarehe 07 Juli 2025

Mbinu za Kutafsiri *Dhulma* (2025), Riwaya Mpya ya Abdulrazak Gurnah

Ida Hadjivayanis

Tafsiri, kama uwanja wa utafiti na utendaji, imekuwa sehemu ya msingi katika historia ya fasihi ya Kiswahili, ikitumika kama chombo cha kuakisi na kudhibiti mitazamo ya kijamii. Katika muktadha wa ukoloni, tafsiri zilihusishwa na juhudi za kulazimisha mitazamo ya kigeni kwa kufanya kazi asili zilingane na mazingira ya Waswahili. Leo hii, tafsiri imechukua nafasi muhimu katika harakati za kurejesha nyumbani kazi za waandishi wa Kiafrika wanaoandika kwa lugha za kikoloni, kama sehemu ya mradi mpana wa udekolonishaji wa maarifa. Wasilisho hili litaangazia jinsi tafsiri ya *Dhulma* (2025), riwaya mpya ya Abdulrazak Gurnah, *Theft*, inavyoweza kusawiriwa kama zoezi la kifalsafa na kisiasa la kuibua, kurejesha, na kusawazisha maarifa ya Kiafrika yaliyodhulumiwa kihistoria.

Ida Hadjivayanis ni Mhadhiri Mwandamizi wa Masomo ya Kiswahili katika SOAS, Chuo Kikuu cha London. Ametafsiri kazi za fasihi kadhaa zikiwemo *Peponi* na *Dhulma* za Abdulrazak Gurnah, pamoja na *Alisi ndani ya Nchi ya Ajabu*. Pia, ameshirikiana na Issa Shivji kutafsiri *Mashairi kwa Walio Hoi*. Yeye ni mwanzilishi wa Baraza la Kiswahili la SOAS linalofanyika kila mwaka.

Kikao kitafanyika **siku ya Jumatatu, tarehe 07 Juli 2025, saa kumi na moja za Ulaya ya Kati** (saa kumi na mbili za Afrika Mashariki) **kupitia njia ya Zoom:**
<https://us02web.zoom.us/j/83474599250?pwd=rrcvQUjTmZ7buqraFjIN7ai1ecaaF8.1>

KARIBUNI NYOTE!

Tafadhalini wajulisheni wapenzi wote wa Kiswahili na marafiki wengine!

Wasalaam,
Kai Kresse, Lutz Diegner na Maxwell Omondi Ondieki

Kama kuna maswali yoyote kuhusu baraza hili tafadhalini mwandikieni mwenzetu:
<MaxwellOmondi.Ondieki@zmo.de >